

## Faida za nyongeza iliyotengenezewa nyumbani

- Kiwango sawa cha ubora kama kile cha dukani
- Rahisi ikilinganishwa na kile cha dukani
- Kinakubaliwa na ng'ombe
- Ni rahisi kutayarisha na kukitumia.



## Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

### Watayarishi:

Muia, J.M.K. na Kariuki, J.N Mbugua, P.N. na Gachuiiri, C.K.

### Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

#### Mkurugenzi wa Kituo,

KARI-Naivasha

S.L.P. 25

Baruapepe: karainav@kenyaweb.com

Simu: 254-050-50483

Vijitabu vya KARI vya taarifa, nambari / 57 /2008

**Shilingi 20 za Kenya**

# Lishe nyongeza ya ng'ombe ya kinyumbani kwa bei nafuu



## Utanġulizi

Ng'ombe anayelishwa nyasi pekee hawezi kufikia upeo wake wa maziwa. Hivyo, kuna haja ya kuwapa nyongeza.

Nyongeza za kununua kama vile chakula cha ng'ombe kinakisiwa kuwa asilimia 20 ya gharama yote ya maziwa na hivyo kupunguza faida ya mkulima. Kutengeneza nyongeza kwa kutumia mali ghafi yanayopatikana kwa urahisi ni chakula kwa bei nafuu na hufanya haziwa kuongezeka na gharama kusalia ya chini.

## Nyongeza ya ng'ombe iliyotengenezewa nyumbani

Ili nyongeza kuwa ya manufaa kwa ng'ombe, sharti iwe na viwango sawia vya nishati, protini na madini.

## Mfano wa chakula chenye nishati ya juu

- Maganda ya mahindi
- Pogoa ya ngano (poladi)
- Molasi
- Kapi za mahindi
- Kapi za ngano.

## Chakula chenye protini nyingi

- Majani ya Lucerne
- Keki za mbegu za pamba

- Maharagwe ya soya
- Keki ya mbegu za alizeti
- Majani ya sesbania
- Chakula cha samaki

## Chemchemi za madini

- Chumvi ya fosfati
- Chokaa
- Fosfati ya mawe
- Madini kabla ya kuchanganyika.

## Jinsi ya kuchanganya nyongeza ya ng'ombe

### 1: Nyongeza ya kawaida

Kutengeneza kilo 100 za nyongeza tumia:

- Kilo 75 za chakula cha nishati/nguvu
- Kilo 23 za protini
- Kilo 2 za madini.

### Mfano

- Kilo 57 za maganda ya mahindi
- Kilo 18 za pogoa ya ngano
- Kilo 17 za Lucerne hifadhi kavu
- Kilo 6 za soya
- Kilo 2 za mbolea ya fosfati.

### 2: Nyongeza ya ngombe ya kiwango cha juu

Ili kutengeneza kilo 100 za nyongeza, tumi:

- Kilo 68 za chakula cha nishati

- Kilo 30 za chakula cha protini
- Kilo 2 za madini.

## Mfano

- Kilo 50 za maganda ya mahindi
- Kilo 16 za pogoa ya ngano
- Kilo 2 za molasi
- Kilo 14 za Kiki ya mafuta ya Pamba
- Kilo 12 za majani ya inserini
- Kilo 4 za chakula cha samaki.

## Gharama

Mkulima huoka hela anapotumbia nyongeza ya kutengenezewa nyumbani badala ya kununua kama ifuatayo:

Kilo 70 kwa gunia	Gharama*	Kuokoa
Nyongeza ya kununua	1,150	-
Cha kawaida cha nyumbani	750	400
Cha hali ya juu cha nyumbani	850	300

\*Bei za chakula ya wanyama wa 2008